# Kulinda miti yako ya parachichi dhidi ya ugonjwa wa kuoza mizizi

Ugonjwa wa kuoza mizizi ni tatizo kubwa katika ukuzaji wa parachichi, lakini hili linahitaji mbinu jumuishi ili kudhibitiwa.
Ugonjwa wa kuoza mizizi unaweza kudhibitiwa kwa Kutumia asidi ya fosforasi mara kwa mara. Asidi inaweza kudungwa au kunyunyuzia, laiki muda wa kutumia dawa ni muhimu sana kuzingatiwa. Asidi ya fosforasi inapowekwa, hutafuta sehemu ya mti ambayo inakua zaidi wakati huo. Kwa kuwa ugonjwa huo huathiri mizizi ya mimea, ni muhimu kutumia asidi ya fosforasi wakati mizizi inakua.

## Asidi ya fosforasi

Asidi ya fosforasi inaweza kutumika kwa sindano au kunyunyiziwa. Njia ya kudunga inaweza kutumika kwa miti iliyo na ugonjwa na ile yenye afya nzuri. Njia ya kunyunyizia inapaswa kutumika kwa miti yenye afya nzuri.
Asidi ya fosforasi haipaswi kamwe kutumika kwenye udongo. Ufanisi bora hupatikana wakati viwango vya uvukizi viko juu na miti ina unyevu wa kutosha.

## Mchakato wa kutumia dawa

Kwa kutumia sindano, asidi ya fosforasi hutumiwa kwa kiwango cha mchanganyiko wa 20% ambao hupatikana kwa kuyeyusha sehemu 1 ya asidi ya fosforasi na sehemu 2 za maji.
Ili kujua kiasi cha asidi ya fosforasi kinachopaswa kudungwa kwa kila mti, kwanza pima kipenyo cha mti na dunga 15ml ya mchanganyiko kwa kila mita ya kipenyo cha mti.
Ingiza 20ml kwa kila shimo la sindano. Chagua maeneo ya kudunga sindano kwa umbali fulani kutoka kwa eneo zilizodungwa awali, na sio juu moja kwa moja ya eneo zilizodungwa sindano awali. Pia epuka kudunga dawa katika makutano ya tawi.
Tofauti na njia ya kutumia sindano, dawa nyingi zinahitajika

ili kuingiza asidi ya fosforasi ya kutosha kwenye mti. Koleo la mchanganyiko wa dawa linapaswa kuwa 0.5%.